

# TIA SAHIHI AHADI

## KWA MGOMBEAJI

► Je wewe ni mgombeaji katika uchaguzi ujao? (wa mwezi Agosti 2022).

Kama uko na hamu na motisha ya kuwakilisha wakaazi wa Mombasa basi ungana na sisi kwa kuambatisha sera zako na matakwa yetu. Kwa maelezo zaidi wasiliana na sisi kwa njia ya barua pepe; okoamombasa@gmail.com.

## KWA MPIGA KURA

► Je unapanga kuwapigia kura wale viongozi ambao wamekubaliana na matakwa yetu na kuyazingatia matakwa hayo kama sera zao.

Piga picha ikiwa umeshikilia nakala hii na uichapishe kwa ukurasa wako wa Twitter ama Facebook na utag Okoa Mombasa ama ututumie barua pepe kupitia: okoamombasa@gmail.com

## JE OKOA MOMBASA NI KINA NANI?

► Okoa Mombasa ni muungano wa vyama vya wafanyakazi, wafanyi biashara, mashirika ya kijamii na wakaazi wa Mombasa, kwa hofu na athari za kuzoroteka kwa hali za kimaisha na uchumi wa Mji wa Mombasa.

Lengo letu kubwa ni kuhakikisha mkaazi wa Mombasa ana husishwa kwa ugavi na matumizi za rasilimali za mji wao.

Tafuta ufahamu zaidi kwa tovuti yetu:  
okoamombasa.org



#OKOAMOMBASA

### WANACHAMA WETU

- Ajenda Kenya
- Dock Workers Kenya
- Fast Action Summit
- Haki Yetu Organisation
- InformAction
- Human Rights Watch
- Kenya Long Distance Trucks Union
- Kenya Transporters Association
  - Mombasa residents
- Muslims for Human Rights
- Taireni Association
- Stella Maris International



[www.okoamombasa.org](http://www.okoamombasa.org)



@OkoaMombasa



OkoaMombasa

# MATAKWA YA OKOA MOMBASA 2022



### MAELEKEZO YA WANASIASA KWA KUWAKILISHA MOMBASA

Mchipuko huu wa Madai haya yametokana na kutowajibika kwa viongozi ambao wamekua waki ahidi na kutotimiza ahadi zao/hizo.

Wakaazi wa Mombasa tunawajulisha kwamba ni bora tuwapigie kura wale viongozi ambao watajitokeza na kuambatisha sera zao na matakwa yetu na ikiwa watapata fursa ya kuchaguliwa tuwe tunaweza kuhakikisha wamewajibika.

# MADAI MANNE KWA MOMBASA BORA

- 1
- 2
- 3
- 4

Kwa uchaguzi unaokuja lazima Mombasa iwakilishwe kikamilifu na wakaazi kupewa kipao mbele.

Tumeorodhesha njia nne mwafaka ambazo tumeona zitafufua uchumi na kuboresha maisha ya wakaazi wa Mombasa.

**Wakazi wa Mombasa** tunawajulisha kwamba ni bora tuwapigie kura wale viongozi amabao watajitokeza na kuambatisha sera zao na matakwa yetu na ikiwa watapata fursa ya kuchaguliwa tuwe tunaweza kuhakikisha wamewajibika.

**Soma maelezo zaidi hapa:**

[www.okoamombasa.org/news/election-pledge-2022](http://www.okoamombasa.org/news/election-pledge-2022)



## DHULUMA ZA KIUCHUMI

Tunapinga maelekezo ya serikali kwamba makasha yote ya kuelekea bara ni sharti yasafarishwe kwa reli ya SGR, hii imedhuru sana Uchumi wa Mombasa na kusababisha upotevu wa ajira.

## KUHUSISHA UMMA

Tunapinga vikali kutohusishwa na serilali kuu kama wakaazi wa Mombasa kwa mwelekeo wa serikali ku kwamba wafanyi biashara wasafirishé mali zao kwa reli ya SGR. Jambo hili limekithiri uchumi wa Mombasa mno.

## UWAZI NA UADILIFU

Tunapinga vile kandarsi ya reli ya SGR ilifanywa kwa njia fiche haswa tukizingatia kwamba serikali ilichukua mkopo ambao makubaliano yake yamefichwa hadi leo

## UGATUZI

Tunapinga sera za serikali ambazo zinahujumu ugatuza, kwa mfano sisi tunaona kwamba Kilindini palipo Halmashauri ya Bandari ya Kenya ni rasilimali ya Mombasa basi inatakikana serikali ya kaunti ya Mombasa kupata mapato kwa njia ya kuwatoza ushuru kwa manufaa ya uchumi wa Mombasa.

1

## VIONGOZI WATUHAKIKISHIE:

- Kwamba watapigania na kubadilisha maagizo hayo ili wakaazi wa mombasa wawe na uhuru wa kuchagua mfumo wa kusafirisha makasha
- Kuwe na njia mbadala ya kutengeneza ajira ili kupunguza athari za walipoteza ajira.
- Kuboreshaji barabara kuu ya Mombasa - Nairobi ili usafirishaji uwe wa kiufanisi na kunogesha biashara kwa jumla.

2

## VIONGOZI WATUHAKIKISHIE:

- Kwamba Wakaazi watahusishwa kwa shughuli zote za ugavi na matumizi za rasilimali za Mombasa.
- Wakaazi Kuhusishwa kwa kupatiwa nafasi ya kutoa maoni kwa jina linalofaa kutajwa hifadhi ya mama ngina, jina litalovutia kihistoria ya Mombasa.

3

## VIONGOZI WATUHAKIKISHIE:

- Kwamba watapigania kuhakikisha kandarsi ya reli ya SGR na Mkopo utawekwa wazi.
- Kwamba waliovunja sheria kuchukuliwa hatua za kisheria.

4

## VIONGOZI WATUHAKIKISHIE:

- Kwamba maslahi ya wakaazi wa Mombasa inapewa kipao mbele na viongozi kuwajibika.
- Serikali ya kaunti kuboresha ugatuza na kupatia kipao mbele sera za ugavi wa rasilimali kwa manufaa ya wakaazi wa Mombasa.